REGISTRY COPY


HAKIARDHI

# ARDHI NI UHAI

ISSN NO. 0856-9495 TOLEO LA 04 Mei - Agosti 2005


# Mapambano ya Umma na Maendeleo ya Jamii

- Masimulizi ya Wazalishaji, wawekezaji, wafadhili, wasomi na wana-NGO's



## NUKUU YA LEO

*Mwenyezi Mungu hakuumba jamii yenye matabaka mawili, tabaka la wawekezaji wenye mtaji na tabaka la wavujajasho bila mtaji. Kwani mtaji huo umetoka wapi kama sio matokeo ya uzalishaji ambao huendelezwa na wavujajasho?*

**KATIKA enzi hizi za utandawazi, soko huria na siasa za ushindani, tunaambiwa, maendeleo maana yake ni kuendeleza uchumi sio umma. Kigezo cha maendeleo ni ukuaji wa uchumi, upanuzi wa barabara, ujenzi wa nyumba za kifahari, umilikaji wa magari ya anasa na ongezeko la supermarkets. Profesa Issa G. Shivji anaelezea zaidi katika makala hii....**

MSINGI wa maendeleo ni mtaji na mwenye mtaji, yaani mwekezaji, ndio msukumo au gurudumu la maendeleo, katika msamiati huo wa Maendeleo nafasi ya umma ni ya maskini ambao hutegemea wafadhili.

Lakini mimi sio mtaalam wa msamiati huo wa kisasa. Kwa hivyo nitaachia hao wataalam wa utandawazi waeleze dhana hizo za uwekezaji na umaskini. Kwa upande wangu, mimi ni mfuasi wa ile lugha iliyokuwa inatambua umma kama ni wa wakulima, wafugaji na wafanyakazi yaani wazalishaji.

Umma huo wa wakulima na wafanyakazi sio maskini au ombaomba Endelea Uk.3

## YALIYOMO


- Tahariri Uk.2
- Ubinafsishaji rasilimali za misitu Uk. 4
- Habari za Kitaifa Uk. 6-7
- Maoni Uk. 7
- Makala ya Kimataifa Uk. 9
- Ushairi, Katuni, machapisho Uk. 10
- Kona ya Sheria, Uk. 11
- Habari katika picha, Uk. 12

**ARDHI NI UHAI ni jarida la Taasisi ya Utafiti na Utetezi wa Haki za Ardhi (HAKIARDHI), ambalo hutolewa mara tatu kwa mwaka.**

Kusudi kubwa ni kuwapa wadau wa Taasisi hii taarifa mbalimbali zinazohusiana na mambo ya ardhi.

**Mhariri**
Yefred E. Myenzi

**Bodi ya Wahariri**
Ng'wanza Kamata - M/Kiti
Abdallah Matata - Mjumbe
Rehema Mfaume - Mjumbe

**Mchapishaji**
Alice Shamge

## UJUMBE WA BODI KWA WASOMAJI

WASOMAJI wa jarida hili mnakaribishwa kutoa michango yenu kwa kuuliza maswali, ushauri, maoni au kwa kuandika makala. (zisizozidi kurasa tatu) zitumwe kwa Mhariri kupitia anuani zifuatazo:

Mhariri:
**ARDHI NI UHAI**
**S.L.P 75885**
**Dar es salaam**

Email:
**info@hakiardhi.org**

**Mchapaji**
Ecoprint Ltd.
Email:
**ecoprint@bol.co.tz**

# TAHARIRI

**'UMOJA ni Nguvu utengano ni udhaifu', hivi ndivyo walisema na kuusia wahenga. Na hili limejidhihirisha nyakati zote katika historia ya binaadamu, hususan pale wanyonge na watu waliokandamizwa walipojaribu kupigania haki, uhuru, na heshima ya utu wao.**

Daima kumekuwa na jitihada za wanaohisi kudhulumiwa, kukandamizwa, kuteswa na kunyanyaswa kujenga umoja na kuutumia umoja huo kama silaha yao kubwa dhidi ya wadhulumu na watesi wao. Vita vya majimaji, miaka mia moja iliyopita, ni mfano mojawapo hai na wenye umuhimu wa kipekee katika historia ya nchi yetu ya juhudi za watu kuungana na kupambana na dhuluma na uonevu wa kikoloni.

Aidha kumekuwa na juhudi za aina nyingine, jitihada za kuwazuia wanyonge kuungana. Aghalabu pale wanyonge wanapokuwa wamefanikiwa kuungana, basi huwepo jitihada za kuwagawa na hivyo kudhoofisha jitihada za wanyonge hao kupambana na uovu na uonevu wanaotendewa. 'Gawanya utawale,' ilikuwa silaha kubwa ya wakoloni wa kiingereza katika Afrika. Leo hii, wenye nguvu - za kisiasa, mamlaka, na fedha hutumia kila aina ya mbinu na vishawishi kuzuia watu wasiungane na kuunganisha nguvu zao kukomesha maovu na dhuruma. Ili waendelee kuishi 'peponi'hapa duniani wenye nguvu wanatambua kuwa silaha yao kubwa na yenye nguvu thabiti ni kuwagawa wanyonge na kuwanyima uongozi kwa kuwanunua au kuwatokomeza viongozi wao kila wachipukapo.

Lakini ilishasemwa na wanazuoni kuwa kila palipo na dhuluma basi huwa kuna pingamizi dhidi ya dhuluma hizo. Kwa hivyo mbinu za wakubwa za kudhoofisha umoja na mapambano ya wanyonge huwa ni jitihada za muda tu kwa vile wakati ukifika huzaliwa kizazi kipya ambacho huhoji iweje watu waishi katika dimbwi la unyonge, dhuluma na uonevu. Hawa, kama walivyokuwa kina Kinjekitile katika nyakati zao, huanzisha na kuamsha ari ya mapambano mapya dhidi ya dhuluma.

Nchi yetu inapita katika nyakati za mabadiliko makubwa ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Ni kweli kuwa wakubwa wanataka kila mtu aamini kuwa mabadiliko haya, hata pale yalipokuwa hayana maslahi kwa wanyonge, yamekuwa na manufaa makubwa kwa kila mtu - mijini na vijijini, maskini na matajiri. Matokeo yake wametumia njia, nguvu na kila mbinu kuushwawishi umma wa 'wasioona'manufaa ya mabadiliko hayo kuyaona. Lakini sauti za kutokubali, hasa kutoka vijijini zimeendelea kusema kuna matatizo na hali kwa ujumla inazidi kuwa mbaya. Sauti za watanzania hawa zimesambaa na zinatoka kwa namna na mtindo tofauti japo ujumbe wake ni ule ule - kutoridhika na faida zinazotajwa za mabadiliko, hasa ya kiuchumi, hapa nchini. Wananchi kwa namna moja au nyingine wanasema wana macho, wanatazama lakini hawaoni.

Hata hivyo kelele na dukuduku za wananchi zitaendelea kupuuzwa na kutotiliwa maanani kwa vile tu hazitolewi kwa umoja. Ni kweli zimekuwepo jitihada za kuunda umoja na nguvu za pamoja miongoni mwa makundi mbalimbali ya jamii. Lakini bado jitihada hizo hazijazaa vuguvugu lenye nguvu na mshikamano unaotakiwa kuleta mabadiliko ya msingi yatakayoanza kutoa matumaini kwa 'mafakiri', na kwa namna endelevu kuanza kuyabadili maisha ya mfanyakazi wa ujira mdogo, mkulima na mfugaji wa Tanzania. Kazi ingali pevu na kwa namna yoyote ile haiwezi kufanikiwa kama haitaongozwa na jitihada za kuunda umoja na mshikamano ndani ya vuguvugu lenye lengo la kuleta uhuru na ustawi kwa mafukara wa nchi hii.

# Mapambano ya umma na maendeleo ya jamii

*Inatoka uk. 1*

wakisubiri fadhila za Asasi zisizo za Kiserikali (NGOs) na Lions au Rotarians), bali ni wapiganaji na wakombozi wa jamii yao, wa nchi yao na taifa lao.

Na hiyo sio dhamira yangu binafsi au ndoto za itikadi za kale bali ni ukweli wa kihistoria ambao umedhihirishwa na unaendelea kudhihirishwa bila kujali itikadi za kibwanyenye.

Mimi siko tayari kugeuza wajenzi wa historia na wasanii wa ukombozi kuwa maskini, wala siko tayari kutumia utaalam na usomi wangu kuwadhalilisha wazee wangu, mama zangu, kaka na dada zangu kuwa maskini na mimi niwe 'consultant' wa kupunguza au kuondoa umaskini. Niko radhi kuwa mwanafunzi wa Maendeleo na mapambano! Tukipenda tusipende, tukitaka tusitake, wanyonge ndio wakombozi.

Wazalishaji wameendelea na wanaendelea kulinda utu na heshima zao na kupambana ili kuboresha hadhi yao na maisha yao bila kujua msamiati wa 'haki za binadamu', bila kushiriki katika siasa za ushindani na bila kujali ufadhili wa {NGO's} hakuna jamii yoyote duniani ambayo inaweza kujiendeleza katika uhuru kwa kutegemea wafadhili na wawekezaji. Uwekezaji ni matokeo ya uzalishaji na sio kinyume chake.

Mwenyezi Mungu hakuumba jamii yenye matabaka mawili, tabaka la wawekezaji wenye mtaji na tabaka la wavujajasho bila mtaji. Kwani mtaji huo umetoka wapi kama sio matokeo ya uzalishaji ambao huendelezwa na wavujajasho? Ni mfumo wa unyonyaji uliojengeka kihistoria ambao hufanya wazalishaji wasiwe walimbikizaji wa mtaji na wasio wazalishaji ndio huwezeshwa kulimbikiza mtaji. Sio nia yangu leo hii kuzungumzia nadharia au historia ya mifumo ya unyonyaji. Ninachotaka ni kusisitiza tu, bila aibu wala bila kusita, kwamba katika historia ya binadamu na historia ya nchi yetu wazalishaji wenyewe ndio wameendeleza na wanaendeleza mapambano ya ukombozi. Nitagusia mifano michache tu.

## Mapambano ya Hanang

Mnamo miaka ya 70, wakazi wa Hanang ambao hujulikana kwa jina la Barbaig, ingawa wao wenyewe hujiita Wadatoga, walijikuta katika Operesheni hiyo iliyowakusanya Wabarbaig katika vijiji. Kijiji kimojawapo ambacho kilikuwa kijiji cha asili na baadae kikaandikwa rasmi chini ya Sheria ya Uandikishaji wa Vijiji ya mwaka 1975 kilikuwa kijiji cha Mulbadaw.

Mwishoni mwa miaka ya 70, ardhi ya Mulbadaw ikavamiwa na NAFCO, Shirika la "umma" au kwa usahihi zaidi tunaweza tukaliita shirika la serikali. Hizi zilikuwa enzi za mashirika ya serikali. NAFCO ilikuwa shirika mojawapo na lilikuwa linasimamia mradi wa ngano kwa msaada wa serikali ya Canada kupitia CIDA.

*Mimi siko tayari kugeuza wajenzi wa historia na wasanii wa ukombozi kuwa maskini, wala siko tayari kutumia utaalam na usomi wangu kuwadhalilisha wazee wangu, mama zangu, kaka na dada zangu kuwa maskini na mimi niwe 'consultant' wa kupunguza au kuondoa umaskini. Niko radhi kuwa mwanafunzi wa Maendeleo na mapambano! Tukipenda tusipende, tukitaka tusitake, wanyonge ndio wakombozi.*

Basi mradi wa ngano ukabuniwa. NAFCO ikapewa maelfu ya ekari ya ardhi bila kujali haki za wenyeji. Mameneja wa NAFCO walitokea sehemu nyingine za nchi na wala hawakuwa na chembe ya uchungu kuhusu hali ya wenyeji.

Nyumba za wanavijiji zilichomwa, mazao yao yakafukiwa chini ya ardhi na matrekta ya NAFCO, mifugo yao ikasambaratishwa, vijana wao wakabuniwa kesi za jinai na kushitakiwa mahakamani, utu wao ukadhalilishwa na askari wa kutuliza ghasia (FFU) na nyumba zao zikapekuliwa kana kwamba za wahalifu.

Siku hizi Hanang ni kituo kimojawapo cha mashirika yasiyo ya kiserikali. NGOs za haki za binadamu hutua Hanang kuwafundisha na kuwaelimisha "maskini" kuhusu haki zao na demokrasia ya vyama vingi, maarifa ya kupunguza umaskini, ustaarabu, usawa wa kijinsia, mfumo mpya wa umilikaji ardhi, na mambo mengine.

Ili mradi kuna hela za wafadhili sisi wakereketwa wa NGOs hatuchoki! Hayo yote yanatufanya tujigambe bila hata kuwa na chembe ya hekima au uzoefu wa umma wenyewe. Ukweli ni kwamba Wabarbaig wana historia ndefu tu ya mapambano dhidi ya dhuluma, ukandamizwaji, uporaji wa ardhi na rasilimali zao.

Mnamo mwishoni mwa miaka ya 70 nilibahatika kukutana na kiongozi wao mmojawapo, Mzee Duncan. Mzee Duncan alikuwa anahudhuria masomo ya viongozi katika Chuo cha Chama Kivukoni. Wakati ule Mzee huyo alikuwa mkereketwa wa Chama. Ninafurahi kwamba anaendelea na mapambano na leo hii yeye kama mwanachama wa HAKIARDHI yupo miongoni mwetu.

Nimesema umma wa Barabaig na viongozi wao walitumia njia mbalimbli za mapambano. Wakaenda katika ofisi za Chama na serikali katika ngazi za tarafa, wilaya, mkoa na taifa. Wakaandika barua za malalamiko kwa Mkuu wa Mkoa na Waziri Mkuu na hatimaye kwa Mwalimu Nyerere mwenyewe. Viongozi wa serikali katika ngazi za Wilaya, Mkoa, na mameneja wa NAFCO kutokana na maslahi yao binafsi, wakawatesa na kuwasumbua viongozi. Mzee Duncan mwenyewe. akasumbuliwa kupita kiasi. Walimu wa shule za msingi ambao walikuwa wanatetea umma wao wakahamishwa na kupewa onyo kali. Wengine wakapoteza ajira zao.

Hatimaye, kijiji cha Mulbadaw na wakazi wengine 66 wakafungua kesi Mahakama Kuu dhidi ya NAFCO. Katika hatua ya kwanza wakashinda lakini NAFCO ikakata rufaa katika Mahakama ya Rufaa. Katika uamuzi ambao ulitegemea mno vigezo vya kiufundi ukatoa ushindi kwa NAFCO. Lakini huo haukuwa mwisho. Umma wa Barabaig wameendelea na mapambano yao.

Mnamo 1986-87, msomi mwenzangu Dk. Ringo Tenga na mimi, tukaenda Hanang kufanya utafiti. Nia yetu haikuwa kujiendeleza kisomi tu bali ni kutoa mchango wetu angalau mdogo katika kutangaza mapambano ya

*Endelea Uk.5*

MAKALA

# Ubinafsishaji wa Msitu wa Longuza: Nani anafaidika?

Na Mwandishi wetu

**DHANA na utekelezaji wa Sera za ubinafsishaji wa rasilimali mbalimbali hapa nchini imezua mjadala wenye maswali na hoja mbalimbali zinazokinzana.**

Aidha kumekuwa na upinzani wa waziwazi dhidi ya sera hizo toka kwa makundi mbalimbali. Hata hivyo Serikali imepuuza na kutozingatia hoja zilizopinga ubinafsishaji wa mashirika ya umma uliofanyika katika mwongo takribani mmoja uliopita. Katika kuimarisha na kuendeleza sera zake Serikali sasa imeingia katika eneo jingine la ubinafsishaji, hili ni eneo linalohusisha mali asili za nchi kama vile ardhi na misitu.

Hivi karibuni Chama cha Wanataaluma ya Misitu walifichua mipango ya Serikali ya kutaka kubinafsisha moja ya misitu yenye thamani ya mabilioni ya shillingi kwa bei ya kutupwa na kwa taratibu zisizozingatia sheria. Toka kuibuka kwa suala hili kumezuka mjadala juu ya mantiki, msukumo, faida, na hasara za uamuzi wa Serikali za kubinafsisha Msitu wa Longuza wilayani Muheza mkoani Tanga. Ifuatayo ni Taarifa ya Tanzania Forestry Association (TAF), inayoeleza kwa nini wanataaluma hawa hawakubaliani na suala la ubinafsishaji wa msitu huu, na vilevile taratibu zinazotumika kuubinafsiha msitu huo. Msimamo huu uliwasilishwa kwenye majadiliano ya wazi yaliyofanyika HAKIARDHI mnamo tarehe 13 Agosti 2005 na baadaye kwenye Semina za Wiki za Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP):

### Hatua za mabadiliko katika sekta ya misitu

Mwaka wa 1998 Serikali ilipitisha sera ya misitu nchini baada ya kupitia ile ya zamani ya mwaka 1953 na kuifanyia marekebisho. Pia mwaka 2002 Bunge lilipitisha sheria mpya ya misitu kwa kuzingatia yaliyomo katika sera ya 1998. Sheria hii ilianza kutumika Julai 2004. Mwaka 2002 programu ya kuendeleza misitu nchini iliandaliwa kama mpango kabambe wa kutekeleza Sera ya Misitu ya 1998. Kufuatia kupitishwa programu ya kuendeleza misitu nchini, Idara ya Misitu na Nyuki kwa msaada kutoka Benki ya Dunia, iliandaa mradi wa Kuhifadhi na kuendeleza Misitu nchini (Tanzania Forest Conservation and Management Project-TFCMP). Baada ya maandalizi na mradi kukamilika ulifanyiwa tathmini na kuonekana unafaa kwa ajili ya kupata mkopo nafuu. Ndipo Benki ya Dunia ilikubali kuikopesha Tanzania dola za Kimarekani. 31.1 million na utekelezaji ulianza mwaka 2002. Mradi wa kuhifadhi na kuendeleza misitu nchini (TFCMP) unashughulikia maeneo makuu matatu:

- Kuazisha Wakala (Executive Agency) kwa upande wa Sekta ya Misitu na Nyuki;
- Kuandaa utaratibu (Private Sector Involvement Framework) utakaotumiwa ili kuhusisha sekta binafsi katika harakati za kutunza na kuendeleza misitu nchini;
- Kuhifadhi na kuendeleza misitu na bioanuai iliyopo katika Milima ya Tao la Mashariki mwa Tanzania (Eastern Arc Mountain Forests Conservation Strategy).

> *...Shamba la Longuza ni chaguo la Viongozi wa Wizara na hakuna sababu za kitaalaam au zenye uzito wa kuridhisha kwa nini liwekwe chini ya sekta binafsi. Hatuelewi kwa nini KVTC inaomba ipewe kuendesha shamba hilo wakati si moja ya mashamba yaliyopendekezwa kwa kufuata vigezo vya kitaalaam....*

Hadi sasa TFCMP inaendelea vizuri na azma yake ya kufanikisha hayo mambo matatu:

- Kwanza, mchakato wa kuanzisha Wakala wa Misitu (Tanzania Forest Services-TFS) ulianza mwaka 2002 na uko katika hatua za mwisho.
- Pili, uandaji wa mkakati wa kutuwezesha kuhifadhi misitu na bioanuai katika Milima ya Tao la Mashariki mwa Tanzania unaendelea vizuri.
- Tatu, utayarishaji wa *kiunzi mhimili* "framework" kitakachotumika kuhusisha sekta binafsi katika sekta ya misitu unaandaliwa.

Kusudi la maelezo haya ni kutoa ufafanuzi: kwanini TAF haikubaliani na utaratibu unaotumiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii (WMU) katika suala zima la kukodisha msitu wa miti aina ya mitiki wa Longuza (Longuza Teak Plantation - LTP) kwa KVTC.

### 3. Kwa nini TAF haikubaliana na Utaratibu wa Kukodisha Msitu wa Mitiki wa Longuza kwa Kampuni ya Kilombero Valley Teak Company?

**Kwanza**, Utaratibu wa kuhusisha sekta binafsi bado unaandaliwa kupitia mradi wa TFCMP. Katika mchakato huo ameajiriwa "Consultant" (Mr. Campbell Day kutoka Norway) tena analipwa mamilioni ya fedha kwa mwezi ili asaidie kukamilisha utaratibu huo. Chini ya mpango huo miradi 5 ilichanguliwa ili iwe kwa majaribio. Miradi hii ni **Sao Hill, Meru, Rongai, Buhindi** na **Kiwira**. Vigezo vilivyotumika kuchagua miradi hii ni pamoja na suala la kushindwa kutekeleza shughuli za kitaaluma mfano kupunguza idadi ya miti, kupogoa matawi, kuotesha miche bustanini na baadaye kuipanda, kutunza barabara hasa za kuzuia moto (fire lines). Haya ni baadhi tu ya matatizo, sasa ilionekana kama sekta binafsi itashirikishwa kutakuwepo na thamani (value) ya kufanya hivyo. Shamba la miti la Longuza halikuhusishwa kwa sababu hakuna thamani itakayopatikana kwa sekta binafsi kushirikishwa huko. Hii ni kwa sababu sehemu kubwa ya shamba miti imekomaa haihitaji huduma zaidi isipokuwa inasubiriwa kuvunwa tu.

**Pili**, Shamba la Longuza ni chaguo la Viongozi wa Wizara na hakuna sababu za kitaalaam au zenye uzito wa kuridhisha kwa nini liwekwe chini ya sekta binafsi. Hatuelewi kwa nini KVTC inaomba ipewe kuendesha shamba hilo wakati si moja ya mashamba yaliyopendekezwa kwa kufuata vigezo vya kitaalaam kama vilivyoelezwa hapo juu. Endelea Uk.8

# Mapambano ya umma

Inatoka uk. 3

wakulima na wafugaji wa Barabaig dhidi ya dhuluma na uporaji wa ardhi yao na vyombo vya dola na tabaka-tawala. Makala yetu ikachapishwa katika jarida la *Africa Events*. Sisi wasomi labda tumechoka, au tumeingia katika ubia Hivi sasa NAFCO iko katika pilika pilika za kubinafsishwa. Kilio cha umma wa Barabaig ni kwamba warudishiwe ardhi yao ambayo ilichukuliwa kutoka kwao bila mashauriano. Ni haki yao. Lakini katika enzi hizi za ubinafsishaji, madai kama haya, ingawa ni ya haki kabisa, hayaingii akilini mwa watawala wachwara. Je, wanaohubiri haki za binadamu wanafanya nini kuhusu madai ya umma?


### Maasai wa Ngorongoro

Mnamo mwaka wa 90, mwenzangu mwanasheria Dkt. Kapinga na mimi tulifanya utafiti kuhusu haki za Wamaasai waishio katika Hifadhi ya Ngorongoro. Hifadhi ya Ngorongoro inajulikana dunia nzima na ina vivutio vikubwa kwa watalii. Mamlaka ya Ngorongoro ambayo ni chombo cha serikali yanakusanya mamilioni ya dola kila mwaka; ni tajiri sana lakini wakazi wa Ngorongoro ni maskini wakutupa.

Katika utafiti wetu tumekuta kwamba mapambano ya Wamaasai yamekuwa ya muda mrefu tangia wakati wa ukoloni. Wamaasai waishio katika eneo la hifadhi ya Ngorongoro walihamishwa kutoka Serengeti na serikali ya ukoloni isipokuwa waliahidiwa na Gavana kwamba wangeruhusiwa kuendelea kufuga na kwamba kamwe hawatahamishwa kutoka eneo hilo. Tangu enzi zile mpaka leo Wamaasai wameishi katika hifadhi kwa wasiwasi kwa sababu mamlaka mbalimbali zimekuwa na dhamira ya kufanya Ngorongoro iwe hifadhi tu bila shughuli za kilimo na ufugaji. Kilimo kimepigwa marufuku na ndio sababu mojawapo iliyosababisha njaa.

Utafiti wetu ulionyesha kwamba Mamlaka ya Ngorongoro ina madaraka makubwa ambayo ni sawa na madaraka ya kiserikali. Mamlaka ina madaraka ya kutunga sheria, kutenda na kuhukumu. Hata hivyo wakazi wa Ngorongoro hawana uwakilishi wa maana katika mamlaka kwa sababu wajumbe wa mamlaka huteuliwa na Serikali na sio viongozi wa kuchaguliwa.

Inajulikana kwamba Mamlaka ya Ngorongoro, ikiungwa mkono na serikali, ina nia ya kuwahamisha wakazi hao ili Ngorongoro iwe hifadhi halisi. Katika dhamira zao hizo Wamaasai wanasumbuliwa na haki zao za kuishi



*Aku Gembul Mpambanaji na mwanaharakati wa haki za Wabarbaig*

kama wananchi zinabanwa. Lakini wazee wa Kimaasai wakitumia busara zao na uongozi wa kijadi wameendelea kupambana.

Inajulikana kwamba katika enzi hizi za uwekezaji anaweza kutokea mwekezaji atakaebuni labda ubia na Mamlaka katika kuendesha hifadhi kwa ufanisi na faida kubwa, ambavyo ni vigezo vya maendeleo katika enzi hizi za soko huria. Ikitokea hivyo, wakazi wa Ngorongoro wanaweza wakapoteza makazi yao. **Je, wakereketwa wa NGOs wana mkakati gani kutoa mchango wao katika mapambano ya umma ya Ngorongoro?**

### Wana wa Rufiji wanusurika

Katika Rufiji wa Delta, mwekezaji kutoka Ireland, akabuni mradi wa kufuga kamba. Ardhi nzuri tu ya wana wa Rufiji ambao huishi kama wavuvi ilichukuliwa na serikali kwa ajili ya mradi huo. Warufiji wakafuata nyayo za babu zao kina Kinjekitile kupambana na uporaji wa ardhi yao. Wakisaidiwa na vijana wanasheria Wanarufiji wakafungua kesi mahakamani. Kabla ya kesi kusikilizwa, waliweza kupata amri ya muda ya kumzuia huyu mwekezaji asiendelee na mradi wake.

Pamoja na kesi, Wanarufiji kupitia viongozi na mashirika yao, na kusaidiwa na HAKIARDHI, wakaendeleza mapambano katika magazeti na vyombo vingine vya habari. Hatimaye, mradi huo ukafa kwa sababu mwekezaji hakuweza kupata mkopo kutoka Ulaya ambao alikuwa anautegemea.

### Hitimisho na Mwanzo

Kwa hiyo mapambano yanaendelea. Mapambano yanaendelea ingawa mazingira ya kisiasa na uchumi yamebadilika. Ukombozi umekuwa mageuzi; wakulima na wafanyakazi wamekuwa maskini; wanyonyaji wamebatizwa jina jipya la wawekezaji; ubeberu unaheshimika kwa jina la utandawazi; mtaji, na sio jasho, ni msingi wa maendeleo. Watafiti na wasomi tumegeuka kuwa wabia, au makuwadi wa wafadhili; wanasiasa wamekuwa wachuuzi wa rasilimali ya nchi.

**Sisi wasomi na wakereketwa hatuna budi kujifunza kutokana na mapambano ya wananchi wenyewe.** Jukumu letu ni kuyatangaza mapambano hayo; kuyasaidia kwa utafiti na usomi, kubuni njia na mbinu mbalimbali za mapambano; kuelewa na kuelewesha nadharia na historia ya mapambano na kubuni mfumo na taratibu mbadala za kujenga uchumi na jamii ambayo itakidhi matakwa na maslahi ya wazalishaji!!!!

## MABADILIKO YA MFUMO WA MILKI YA ARDHI NCHINI.....

# MVIWATA watoa tamko

- ***Wasema yanahatarisha uhakika wa milki kwa wazalishaji wadogo***
- ***Wahimiza kudai, kutetea, kulinda na kushinikiza upatikanaji Haki***

*Na Mwandishi wetu -Morogoro*

**MTANDAO wa vikundi vya wakulima wadogo wadogo nchini ujulikanao kama MVIWATA wenye makao yake makuu mjini Morogoro, hivi karibuni umetoa Tamko kuhusu kasi ya mabadiliko ya mfumo wa milki na matumizi ya ardhi nchini, kuwa inahatarisha uhakika wa milki ya ardhi kwa wazalishaji wadogo hususan waishio vijijini.**

Tamko hilo ambalo lilikabidhiwa kwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro Ndugu Daudi Mfangavo, liliainisha matatizo mbalimbali, ambayo yamekuwa yakiwakabili wakulima na wazalishaji wengine wadogo.

Matatizo hayo ni pamoja na kuporwa ardhi yao na wenye vipato vikubwa, uelewa mdogo wa watendaji wanaosimamia Sheria za ardhi na hivyo kusababisha migogoro isiyo ya lazima, rushwa na kukosekana kwa ulinzi wa uhakika wa rasilimali za wanyonge kama ardhi, misitu, madini, n.k.
Tamko lilitolewa kama sehemu ya majumuisho ya warsha ya mafunzo kwa viongozi wapatao 60 wa ngazi ya Taifa na ngazi ya kati ya mtandao huo ambayo ilifanyika kuanzia tarehe 17 hadi 19 Agosti mwaka huu katika majengo ya Chuo Kikuu cha Waislamu mjini Morogoro.

Washiriki hao ambao walitoka katika mikoa na wilaya zaidi ya 18 za Tanzania bara na visiwani walijumuisha kanda zote tisa za MVIWATA, walipata fursa ya kujifunza jumla ya mada saba, ambazo ziliwasilishwa na wakufunzi kutoka Taasisi ya Utafiti na Utetezi wa Haki za Ardhi HAKIARDHI, yenye makao yake makuu jijini Dar es Salaam.

Mada hizo zilihusu misingi na upatikanaji wa haki katika mifumo ya kidemokrasia, haki za ardhi kwa wazalishaji wadogo wadogo kwa mujibu wa sera na Sheria za ardhi pamoja na mifumo mbalimbali ya utatuzi wa migogoro ya ardhi na rasilimali nyinginezo.

umma wa Watanzania kwa njia mbalimbali, ili watambue haki zao katika ardhi na hatimaye waendeleza harakati za madai ya mfumo mbadala utakaozingatia haki, maslahi na mahitaji halisi ya wakulima, wafugaji na makundi mengine ya wanyonge kote nchini.

Tamko hilo lenye vipengele kumi limeweka bayana kuwa, mustakabali wa nchi hii bado utaendelea kuwategemea wakulima na wafugaji wadogo wadogo. Hivyo hatua zozote za serikali inayojali ustawi na maslahi ya muda mrefu ya Watanzania haina budi kuwekeza vya kutosha na ipasavyo katika sekta ya wakulima wadogo wadogo.

Pia limeeleza kuwa, Sheria za ardhi za Mwaka 1999 na marekebisho ya Mwaka 2004 hayakidhi haja ya madai ya wakulima vijijini kuwa na uhakika madhubuti wa ardhi yao. Kwa hivyo, Sheria za ardhi hazina budi kufanyiwa mabadiliko ya msingi kutoa uhakika wa milki ya ardhi, ili kuwawezesha wananchi vijijini kupambana na mikikimikiki ya soko huria.

Hali kadhalika, utaratibu wa usambazaji wa gazeti la serikali ambalo hubeba taarifa muhimu zenye athari kwa wakulima vijijini hauna budi kuangaliwa upya. Hii ni kwa sababu magazeti hayo huwa hayafiki vijijini na maamuzi yanayowaathiri wananchi hufanywa kwa kuchukulia kwamba wananchi wamepatiwa taarifa husika. Kwa hivyo Serikali ihakikishe kuwa magazeti hayo yanasambazwa mpaka vijijini.

Vile vile, sera na sheria za ardhi zinazoruhusu wachache kujilimbikizia ardhi ni hatari, kwanza zinachangia katika kudumisha na kufukarisha walio wengi vijijini na kuhatarisha amani na utulivu wa nchi kwa siku zijazo.

Pamoja na mapungufu ya kisera na kisheria, Serikali haina budi kuheshimu na kusimamia sera Sheria na taratibu za ardhi, kwamba imedhihirika kuwa watendaji wa Serikali ndiyo wamekuwa wavunjaji wakubwa wa Sheria na taratibu na hivyo kupokonya wananchi haki na kuchochea migogoro.

Aidha uhamasishaji unaofanywa na serikali kuwataka wakulima maskini kuwa na hati miliki za ardhi na kuzitumia hati hizo kama dhamana ya mikopo kwenye mabenki ya kibiashara hauna budi kuangaliwa kwa tahadhari kubwa kwani mabenki ya biashara hayana nia dhahiri ya kukopesha wakulima maskini, bali pia pale yatakapofanya hivyo lengo lao litakuwa ni Endelea Uk.7



*Mafunzo ya sheria za Ardhi vijijini, kata ya Magole wilayani Kilosa yakiendelea chini ya uratibu wa Haki Ardhi hivi karibuni.*




*Mwanaharakati Murisa Tendai toka Zimbabwe akitoa mada hivi karibuni katika kongamano la Haki za Ardhi lililofanyika nchini, katikati ni Mwenyekiti wa Kongamano hilo Mzee Emmilian Jaka na kulia ni Mratibu Bw. Yefred Myenzi*

# MVIWATA watoa tamko

*Inatoka uk. 6*

kujilimbikizia ardhi kwa ajili ya kuiuza kwa faida ya siku zijazo.
Pia, Serikali inalo jukumu na wajibu wa kuanzisha mifuko ya mikopo kwa wakulima wadogo, mikopo ambayo itakuwa yenye masharti nafuu, na ambayo haitalazimisha wakulima kutumia ardhi kama dhamana na badala yake mazao ndiyo yatumike kama dhamana.

Vilevile limebainisha kuwa, sera na mikakati ya Serikali inayotoa kipaumbele kwa wawekezaji wakubwa, hususan wa ndani na wa nje, katika sekta ya kilimo haizingatii athari za muda mrefu za mikakati hiyo ambayo ni pamoja na kuwageuza wakulima wadogowadogo vijijini, kuwa watwana.

Limeeleza kwamba, mfumo wa uchumi wa soko huria unaoruhusu uingizaji bidhaa za kilimo toka nje ya nchi ni hatari kwa nchi kwani unahatarisha maisha, ustawi na maendeleo ya wakulima wadogo wadogo. Hivyo Serikali inao wajibu wa kukuza na kulinda masoko ya ndani ya bidhaa za kilimo, na kwa kushirikiana na asasi za wakulima wadogo kutafuta masoko ya bidhaa hizo nje ya nchi.

**"Ni muhimu pia wakulima na wafugaji wadogo wadogo kutambua kuwa wanalo jukumu la kudai, kutetea, na kulinda haki zao kupitia vyombo vyao wenyewe, taasisi na vyombo vya maamuzi vya kiserikali vyenye uwakilishi na kwa kushirikiana na wadau wengine" limeeleza Tamko hilo.**
Tamko hili ni sehemu tu ya jitihada ambazo vikundi vya kiraia vimekuwa vikifanya, ili kuhakikisha kuwa mfumo wa milki ya ardhi nchini unamnufaisha mwananchi wa kawaida badala ya kumgeuza kuwa mtumwa katika nchi yake mwenyewe.

Itakumbukwa kwamba MVIWATA ilitoa Tamko jingine kupinga matumizi ya mbegu zenye viini tete, zijulikanazo kitaalamu kama GMOs.

Jitihada hizi hazina budi kuungwa mkono na jamii nzima kwani asasi hizi za kiraia ni chachu tu ya mabadiliko, au mwangwi wa sauti lakini sauti yenyewe ni ya jamii nzima.

Hivyo ni vema kila mwanajamii akapata shauku ya kushiriki kikamilifu na hatimae kuchukua jukumu kama wanaharakati hao wa MVIWATA walivyotoa shime, katika hitimisho la Tamko lao kuwa; kila mmojawetu abebe jukumu la kudai, kutetea, kulinda na kushinikiza upatikanaji wa haki yake kupitia asasi za kijamii na kiraia, vyombo vya maamuzi vya serikali vyenyewe uwakilishi na kwa kushirikiana na wadau wengine.

# MAONI

**Ndugu Mhariri,**
KWA kuwa gazeti la HAKIARDHI huwaelimisha wananchi walio wakulima na wafugaji wadogo wadogo nchini, mimi naomba gazeti hili lisambazwe sehemu nyingi za vijiji vyetu vya Wilaya ya Kisarawe kwani hivi sasa kumejitokeza matatizo mengi ya watu wachache wenye fedha kupora ardhi za babu zetu na kumiliki maeneo ya hekari nyingi bila ya kuwahusisha wahusika.

Hivyo magazeti na vitabu vitasaidia wanakijiji kufahamu haki zao na nini cha kufanya na kufahamu nchi kwa hivi sasa inakwenda katika mfumo gani!
Mohamedi Betela (Pingu).
**S.L.P. 28000,**
**(W) Kisarawe, Mkoa wa Pwani.**

**Ndugu Mhariri,**
HAKIARDHI ni chombo cha Wanyonge kinachowaunganisha wanavijiji wa kulima na wafugaji wadogowadogo wanaodhulimiwa haki zao na wajanja wachache tuliowachagua na kuwaweka madarakani. Hivyo natoa pongezi sana kwa timu nzima ya HAKIARDHI kwa kuendesha mapambano ya kutetea haki zetu sisi wakulima wa hapa Buyuni na maeneo mengine ya nchi. Hivyo naomba Taasisi ikiwezekana iandae kitabu cha Buyuni chenye kuonyesha harakati za mapambano ya kudai haki za wanakijiji dhidi ya serikali ya awamu ya tatu ilivyokuwa, ili kitabu hicho kiwe ni historia kwa watoto wetu na wajukuu zetu.
**Nashukuru kwa kupata Gazeti**
**Bi Fatuma Mohamedi (Mama Nuni)**
**Buyuni**

**Ndugu Mhariri,**
NASHUKURU sana kwa kupata nakala ya Gazeti hili. Napendekeza gazeti hili liendelee kutolewa ili iwe changamoto kwa sisi wanyonge tunaosulubika na maisha ya kila siku, huku hao wakubwa wakiendelea kuneemeka bila nasi kutujali kama watu ambao tunahitaji maisha mazuri. Ubinafsi na uchu wa kipato cha haraka haraka kwao unasababisha kutunyang'anya kidogo tulichokuwa nacho sisi wakulima wadogo bila ya kufuatia Sheria hizo walizopanga wao wenyewe. Roho yangu inauma sana pale hawa wenye madaraka kutunyang'anya ardhi ndogo tuliyopewa na operesheni vijiji bila ya aibu, watu hawa ni hatari sana kwa maisha yetu. Wanavijiji popote pale nchini tuwe macho na watu hao.
**Ahsante**
**Mimi Dorisi Mkopi**

MAKALA

# Ubinafsishaji wa Msitu wa Longuza: Nani anafaidika?

*Inatoka uk. 5*

**Tatu**, Shinikizo la Wizara kwa wataalaam wa misitu kwamba watayarishe mkataba wa kutoa shamba hilo kwa KVTC linatokana na maombi ya Commonwealth Development Corporation (CDC) na Ubalozi wa Finland ambao ndio wenye kumiliki KVTC. Kwa nini wanataka shamba hilo na si mojawapo kati ya matano yaliyotajwa katika aya (1), wanajua fika kuwa wakipewa kampuni yao itapata faida sana. Kwa nini Watanzania wenyewe wasipate faida hiyo?

**Nne**, Consultant" wa kufanya "inventory" na tathmini ya shamba hilo alitafutwa na kugharamiwa na Ubalozi wa Finland. Hii ni kinyume kwa sababu ndio wenye KVTC. Gharama zimefanywa za juu sana na mapatao kuwa kidogo. Isitoshe bei ya kuuzia wametumia iliyoidhinishwa na serikali (yaani Tshs. 50,000.00 kwa $m^3$ moja badala ya bei ya soko ambayo kwa wanunuzi wa hapa Tanzania si chini ya Tshs. 140,000.00 kwa $m^3$ moja. Lakini wao wakiuza itakuwa zaidi ya kiasi hicho.

> *Katika ujumla wake thamani ya shamba la Longuza ni takribani Tshs. 60 billion kwa miti tuu peke yake ukiacha aina nyingine za miti. Hata kama mwekezeji ataweka fedha zake kule lakini thamani ya Tsh. 7 billion ni ya chini sana.*

**Tano**, Kiasi wanachotaka kutoa cha Tshs. 7 billion ni kidogo sana ukilinganisha na thamani ya miti yenyewe. Kuna zaidi ya hekta 1000 zenye miti zaidi ya miaka 30 tangu ipandwe na hii inaweza kuvunwa. Picha halisi ni: miaka 31-40 ni hekta 1032.5; miaka 41-50 ni hekta 18.8 na zaidi ya miaka 50 ni hekta 31.6 jumla ikiwa hekta 1082.9 kwa ujazo wa zaidi ya 270,000 $m^3$. Thamani yake si chini ya Tshs. 38.7 billion ukiacha mitiki ambayo ni chini ya miaka 30 ambayo ni karibu hekta 440. Katika ujumla wake thamani ya shamba la Longuza ni takribani Tshs. 60 billion kwa mitiki tu peke yake ukiacha aina nyingine za miti. Hata kama mwekezeji ataweka fedha zake kule lakini thamani ya Tsh. 7 billion ni ya chini sana.

**Sita**, Kutayarisha mkataba bila ya kuwepo mwongozo (**Guidelines**) uliokubaliwa kitaaluma na kwa wadau muhimu katika sekta ya misitu na nyuki ni kosa. Concession agreement inatakiwa itayariishwe kulingana na guidelines kinyume cha hapo ni kudhalilisha taaluma ya misitu

**Saba,** Siyo siku nyingi Idara iliuza miti ya mitiki kutoka shamba la Mtibwa lenye meta za ujazo 42,000 $m^3$ na kupata Tshs. 6 billion sasa iweje shamba lenye zaidi ya 400,000 $m^3$ litolewe kwa Tshs. 7 billion tu? Je, tunatoa zawadi kwa CDC na Finland au vipi? Mashamba ya mitii yalipandwa kwa faida ya Watanzania na si vinginevyo kama wananunua twende kwa bei ya soko tena soko la dunia. Uuzaji wa mitiki hiyo utangazwe kidunia

**Nane**, Utaratibu wa kutangaza haujafuatwa ili kutoa fursa kwa wawekezaji wengi wa ndani na nje ya Tanzania kushiriki na hatimaye kumpata mwekezaji ambaye ataleta faida zaidi kwa Watanzania (This fits well into the good governance and transparency requirements). Pia kutangaza kitu kama hiki kunaondoa mazingira ya kutatanisha na hisia za rushwa na dhuluma kwa Watanzania ambao wengi wao ni masikini

**Nane,** Swala lenyewe linashughulikiwa kwa mwendo wa kutisha kiasi kwamba watalaam hawapewi nafasi na muda wa kutosha kufanya kazi vizuri kwa faida ya Watanzania badala yake mambo yanaenda haraka kwa faida ya wachache

**Tisa,** Lugha inayotumika kwamba serikali imekwisha kuamua kwamba shamba la Longuza wapewe KVTC inatisha sana. Je, serikali iliamua kwa kutumia vigezo gani? Kwani shamba la mitiki la Longuza limegeuwa kuwa kiwanda au kampuni ya umma? Si ni shamba la miti ambalo lilipandwa kufuata taratibu za kitaaluma sasa iweje linapofikia kuvunwa taratibu za taaluma zipuuzwe na ushauri wa wataalam usiwe na maana yoyote kwa viongozi wa Wizara? Je hii ni haki kwa wanataaluma?

> **Siyo siku nyingi Idara iliuza miti ya mitiki kutoka shamba la Mtibwa lenye meta za ujazo 42,000 $m^3$ na kupata Tshs. 6 billion sasa iweje shamba lenye zaidi ya 400,000 $m^3$ litolewe kwa Tshs. 7 billion tu? Je, tunatoa zawadi kwa CDC na Finland au vipi? Mashamba ya mitii yalipandwa kwa faida ya Watanzania na si vinginevyo kama wananunua twende kwa bei ya soko tena soko la dunia. Uuzaji wa mitiki hiyo utangazwe kidunia**

Kutokana na hayo yote TAF ilitoa ushauri kwa wizara kwa nia njema kuwa mchakato wa kutoa shamba la mitiki la Longuza usitishwe kwa sababu taratibu za kisheria na taaluma ya misitu hazifuatwi ikiwa ni pamoja na:

**Kwanza**, kutokuwepo **mwongozo** wa kushughulikia maswala ya sekta binafsi (bado unaandaliwa kupitia TFCMP)

**Pili,** Orodha ya rasilimali (Inventory) na uthamini uliofanywa chini ya ufadhili na kuendeshwa na mwenye kampuni haukubaliki hivyo kama ni lazima sana kutoa shamba hilo kwa sekta binafsi **utambuzi wa orodha hiyo na tathmini vifanyike upya.**

**Tatu**, Wizara iko mbioni kuunda TFS (Wakala wa misitu) hivyo mashamba ya mitiki yaachiwe TFS ambayo ikishaanzishwa itaweka utaratibu mzuri wa kuyaendesha ikiwa ni pamoja na kuuza mitiki kwa bei nzuri na kuweka mkakati mahususi wa kuendeleza mashamba pamoja na wananchi wanaoishi karibu na shamba husika."

MAKALA YA KIMATAIFA

# Mapinduzi katika mfumo wa umiliki wa Ardhi Venezuela

Na Emmanuel Mvula

MWEZI Machi 2005, Serikali ya Venezuela inayoongozwa na Rais Hugo Chavez, imeanza kutimiza kampeni yake ya kwanza katika mpango wa kugawanya upya ardhi kutoka wamiliki wakubwa wa ardhi, kwenda kwa wananchi masikini wasio na ardhi nchini humo, ambao wanategemea ardhi hiyo kwa maisha yao.

Mpango huo ni matokeo ya mapambano ya wakulima dhidi ya mfumo dhalimu wa umiliki wa ardhi nchini humo, ambao umedumu kwa karne nyingi. Mfumo huo uliwezesha watu wachache ambao ni matajiri na viongozi wa dola katika awamu mbalimbali za uongozi nchini humo kumiliki na kuhodhi ardhi kubwa.

> *"Historia inaonyesha kwamba toka uvamizi wa Wahispania katika mwaka 1492, 'wananchi wa Venezuela wamekuwa wakipamba na kwa ajili ya usawa, haki na kuondoa unyonyaji. Usawa na haki katika ardhi lilikuwa ni jambo la msingi katika mapambano haya ya kiutu"*

Wengi wa matajiri hao walikuwa ni walowezi na makampuni makubwa ambayo yanamilikiwa na walowezi, mabepari wanaoishi nje ya Venezuela na baadhi yao sio raia wa nchi hiyo, kama vile kampuni ya Vestey Group inayomilikiwa na Sam Vestey, ambaye pia ni mmiliki wa msururu wa machinjio ya Dewhurst ambaye anadai babu ya babu yake alimilikishwa ardhi Venezuela mwaka 1903.

Hivyo nchini Venezuela kabla ya mabadiliko haya asilimia 5 (tano) tu ya wananchi walimiliki robo tatu ($^3/_4$) ya ardhi yote ya Venezuela. Hii iliwaacha watu wengi wa vijijini/mashambani masikini wasio na ardhi na ambao hawawezi kujitegemeza.

Kwa hiyo mapinduzi haya yamelenga katika Kuondoa tofauti hizo. Kufanikiwa kwa mapinduzi ya safari hii kumetokana na ukweli kwamba serikali ya Venezuela imepania kutoa huduma za mikopo, wataalamu wa kiufundi na misaada ya masoko ili kuyafanya mapinduzi haya ya kimfumo yawe na maana zaidi. Kulikuwapo hapo awali na harakati za kubadili mfumo huo, lakini zilishindwa kutokana na sababu mbalimbali.

"Historia inaonyesha kwamba toka uvamizi wa Wahispania katika mwaka 1492, 'wananchi wa Venezuela wamekuwa wakipambana kwa ajili ya usawa, haki na kuondoa unyonyaji. Usawa na haki katika ardhi lilikuwa ni jambo la msingi katika mapambano haya ya kiutu" anasema Braulio Alvarez, mwanaharakati wa haki za wakulima wadogo, na Mkurugenzi wa zamani wa Taasisi ya Ardhi ya Taifa Venezuela.

Lakini sasa chini ya serikali ya Rais Hugo Chavez, wakulima wanarudishiwa sio tu ardhi yao lakini pia haki yao ya kibinadamu na utu wao. Serikali yao inatekeleza sera ambayo inazitambua haki za asili za mababu. Hivyo mapambano ya masikini yameleta mafanikio makubwa katika kupatikana usawa na mabadiliko ya kijamii.

Serikali ya Venezuela inayaita mabadiliko hayo "Mission Zamora" kufuatia jina la Mwanamapinduzi Ezequiel Zamora, mwanamapinduzi wa karne ya 19, ambaye alipigania mabadiliko endelevu ya kimfumo katika umiliki wa ardhi kwa watumiaji wadogo hususani wakulima, na ambaye alionesha chuki ya wazi juu ya tabaka lililokuwa likihodhi ardhi. Mapinduzi ya sasa yalianza kwa kuanzisha Sheria ya Ardhi na Maendeleo ya Kilimo ya 2001, ikifuatiwa na uanzishwaji wa Taasisi mbalimbali kama vile Taasisi ya Taifa ya Ardhi mwaka 2002.

Wakati Venezuela inafanya mapinduzi hayo kuelekea kule ambako Tanzania imekuwa; Serikali ya Tanzania imeonekana ikifanya kinyume chake na kufanya mabadiliko kuelekea kule ambako Venezuela inakimbia. Nchini Tanzania katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa na mabadiliko ya kimfumo ambayo yanapelekea kuunda tabaka la wenye ardhi na wasio na ardhi, hasa kwa kurahisisha unyang'anyi wa ardhi kutoka kwa masikini kwenda kwa wenye vipato, hususani matajiri na viongozi wa dola, huku ukiwaacha Watanzania wengi wakiwa na hofu ya kupoteza ardhi yao.

Serikali imepitisha marekebisho ya Sheria ya Ardhi ya 2004 namba 2, ambapo sasa ardhi tupu imeweza kuuzwa kama kanzu sokoni, kwa kisingizio cha kuweza kutumia ardhi kama mitaji. Katika mabenki ya fedha sasa ardhi inaweza kutumika kama rehani, huku masharti upande wa mabenki yakiwa yamerahisishwa zaidi, ili kuwezesha mabenki hayo kutwaa ardhi hiyo endapo mkopaji atashindwa kulipa.

> *Wakati Venezuela inafanya mapinduzi hayo kuelekea kule ambako Tanzania imekuwa; Serikali ya Tanzania imeonekana ikifanya kinyume chake na kufanya mabadiliko kuelekea kule ambako Venezuela inakimbia.*

Mabadiliko hayo kimsingi yanarahisisha unyang'anyi na uhamishaji ardhi toka kwa wenyeji masikini walio wengi, na kwenda kwa matajiri walio wachache.

# Ushairi

## *Sisi kwa sisi*

*Futeni jazba*
*Tupilieni mbali siasa*
*Hii ni enzi ya Utandawazi.*

*Fungueni milango,*
*Kaeni uchi,*
*Wakaribisheni Waheshimiwa*
*Ma-inzi, Masiafu na*
*Mashoga.*
*Hii ni sera*
*Ya Uwekezaji*

*Acheni kasumba!*
*Kuleni mtama,*
*Kama sio wa kulima*
*Wa GMOs.*
*Hii ni 'zesheni,*
*Ya akina-Watio (WTO).*

*Vueni shuka, na*
*'Haki ya Mungu'*
*Vaeni suti,*
*Kama sio za wazungu wafu,*
*Za waafa wa Irak*
*Huu ni uchumi,*
*Wa AGOA.*


*Piga makofi*
*Vaa shanga*
*Futuru na mbabe,*
*Mfalme wa dunia.*
*Hii ni karne,*
*Ya nyota na milia.*

*Bro', umepitwa*
*Na wakati!*

*Acha fikra.*
*Uza mawazo*
*Funga tai,*
*Ufutie jasho.*
*Andika:*
*'Milavu Anko Sam',*
*Upate lapitopi*
*'mad in USA'.*

**********************

*Issa Bin Mariamu*




# MACHAPISHO

| Na. | Jina la Kitabu | Mwandishi |
|---|---|---|
| 1. | Not Yet Democracy: *Reform land tenure in Tanzania - 1998* | Issa G. Shivji |
| 2. | Ardhi ni Uhai - *1995* | Georgios Hadjivayanis |
| 3. | Mwongozo wa Haki za Ardhi kwa Wananchi wa Tanzania - *2002* | Issa G. Shivji/ Deus Kibamba |
| 4. | Fukuto la Migogoro ya Maeneo na Hatma ya Wazalishaji Wadogo Wadogo Tanzania - *2002* | Aida Isinika (Mhariri) |
| 5. | Msukumo na Harakati za Kubadili Mfumo wa Umilikaji Ardhi Tanzania - *2000* | Ng'wanza Kamata (Mhariri) |
| 6. | Maasai Rights in Ngorongoro, Tanzania - *1998* Kapinga | Issa G. Shivji & Wilbert |
| 7. | Haki za Wamaasai waishio hifadhi ya Ngorongoro *1999* | Issa G. Shivji, Wilbert Kapinga, |
| 8. | Mfumo wa Umilikaji Ardhi Tanzania, *1997* | Issa G. Shivji and Wilbert Kapinga (Wahariri) |
| 9. | Ripoti ya Tume ya Rais kuhusu maswala ya Ardhi - 1994 | Wizara ya Ardhi |
| 10. | Reclaiming the Land | Sam Moyo & Paris Yeros |

## KONA YA SHERIA

# Miliki ya Ardhi Kimila

*Na Emmanuel Mvula*

**KARIBUNI ndugu wasomaji katika kona ya Sheria, kona ambayo inakufafanulia Sheria kwa njia na lugha rahisi ili wewe msomaji uweze kufahamu haki zako kimsingi katika Sheria za ardhi.**

Leo katika safu yetu hii tunazungumzia suala zima la Miliki ya Ardhi Kimila. Kwanza ifahamike kuwa umiliki wa ardhi nchini Tanzania upo wa aina mbili yaani umiliki wa ardhi kwa hati au kama unavyojulikana kisheria "Granted Right of Occupancy" na ule unaojulikana kama Umiliki wa Ardhi Kimila ujulikanao kisheria kama "Deemed Right of Occupancy".

Kwa mujibu wa Sheria za ardhi, ardhi nchini inaweza kupatikana kwa njia zifuatazo, kugawiwa/kupewa na serikali; na hapa ina maana pia ya serikali ya kijiji kwa idhini ya mkutano mkuu wa kijiji; kusafisha pori tupu na kumiliki, kununua; kurithi; kukodi na hata kupewa zawadi. Baada ya kupata ardhi mmiliki anaweza kumiliki kwa namna hizi mbili zilizotajwa hapo juu. Umiliki wa Ardhi kimila au kama unavyojulikama "deemed right of occupancy" ni umiliki wa raia wa Tanzania mwenye asili ya Kiafrika ambaye anatumia au anamiliki ardhi kwa mujibu wa Sheria za Kimila (fungu la 2 la Sheria ya Ardhi Namba 4, 1999).

Swala la kujiuliza ni kwa nini basi ni raia wa Tanzania mwenye asili ya Kiafrika, ndiye anayeweza kumiliki ardhi kimila? Hii inatokana na ukweli kwamba umiliki wa mila unafuata Sheria za mila husika, endapo raia ambae sio wa asili ya Kiafrika atamilikishwa ardhi kimila basi itakuwa ngumu kujua ni taratibu za mila ipi anafuata. Raia wa Tanzania wasio na asili ya kiafrika wanamilikishwa ardhi kwa njia ya Hati yaani "Granted right of Occupancy". Swala la umiliki kimila, kwa raia wenye asili ya Kiafrika, lilijitokeza katika kesi ya **NAFCO Vs. Mulbadaw village** ambapo suala la msingi lilikuwa kati ya mwanavijiji ambao walikuwa wanapinga kuondolewa katika ardhi yao, ambayo walikuwa wanamiliki kimila, ili kupisha Shirika la NAFCO.

Moja ya masuala ya msingi ilikuwa kuona kama kweli wanakijiji wale walikuwa na haki ya kimila kwa mujibu wa Sheria. Kwa mujibu wa Sheria ya ardhi 1923 (Land Ordinance Cap. 113, 1923) umiliki kimila ulikuwa kwa wenyeji. Mahakama iliendelea kujiuliza swali nani ni mwenyeji? Kwa mujibu wa Sheria ya kikoloni mwenyeji ni yule ambaye si mzungu, wala mwenye asili ya Asia lakini haimjumuishi Msomali. Kumbe katika wale wanavijiji (Wabarbaig) kulikuwa na Mwenyekiti ambaye alikuwa Msomali hivyo "wakashindwa" kuthibitisha kwa uthabiti kwamba wao ni wenyeji, wakashindwa katika kesi hiyo.

> *Ikumbukwe pia ardhi yote ya vijiji nchini inamilikiwa kimila. Hivyo basi panapotokea mgongano wa maslahi kati ya mmiliki wa ardhi kimila na yule mwenye hati, na suala likapelekwa mahakamani basi Mahakama itaangalia nani mwenye miliki halali, na kamwe haitachukuliwa kuwa mwenye miliki kimila hana haki na anageuka kuwa mvamizi au au mkaa holela.*

Labda hapa ingefaa kusema kuwa, kwa muhibu wa Sheria mmiliki wa ardhi kimila anatambulika kisheria na pia ana hadhi sawa na umiliki wa ardhi kwa hati Ikumbukwe pia ardhi yote ya vijiji nchini inamilikiwa kimila. Hivyo basi panapotokea mgongano wa maslahi kati ya mmiliki wa ardhi kimila na yule mwenye hati, na suala likapelekwa mahakamani basi Mahakama itaangalia nani mwenye miliki halali, na kamwe haitachukuliwa kuwa mwenye miliki kimila hana haki na anageuka kuwa mvamizi au mkaaji holela.

Suala la mwingiliano wa kimaslahi kati ya mmiliki kimila na yule wa hati linatokea sana pembezoni mwa miji, ambako ardhi inapimwa kutokana na kupanuka kwa miji, na hivyo kumeza/kuchukua ardhi zilizokuwa na zinazomilikiwa kimila kwa mujibu wa Sheria. Suala hili lilijotokeza katika kesi ya **Metuselah Nyagaswa Vs. Christopher Mbote Nyirabu (1985).** Katika Shauri hili Mahakama ya rufaa ilijadili kwa kina haki ya umiliki wa kimila katika eneo ambalo limetangazwa kuwa la mipango miji. Jaji Mustapha wa Mahakama ya Rufaa akaamua kuwa, haki ya umiliki wa ardhi kimila haifutiki na wala mmiliki hawi mvamizi pale eneo linapotangazwa kuwa la mipango miji. Na mwanasheria wa mrufani akatetea kwamba kwa vile Sheria ya ardhi 1923 inatambua miliki zote mbili, basi kuna uwezekano wa miliki zote mbili kuwa na hadhi sawa/bega kwa bega katika eneo la mipango miji.

Lakini katika hukumu hiyo kama ilivyo katika hukumu nyingi za Mahakama ya Rufaa Mahakama, iliacha kutoa hukumu kwa kuangalia jambo la msingi na badala yake likaamua juu ya swala la kiufundi (Technicality), kuwa mmiliki kimila (Metuselah Ngagaswa )ambaye ni mrufani hakufuata taratibu za kisheria (kimila) ambazo zilimtaka pawepo na ushahidi wa Mwenyekiti wa Kijiji, wakati wa mauziano ya ardhi inayomilikiwa kimila. Sharti ambalo mrufani hakulitimiza kwa vile wakati ananunua ardhi hiyo shahidi aliyekuwepo alikuwa ni Mwenyekiti wa CCM - na si Mwenyekiti wa Kijiji, hivyo hakuwa na umiliki halali dhidi ya yule mwenye hati, kwani umiliki haukupita toka kwa muuzaji kuja kwake kutokana na ukiukwaji wa taratibu za Sheria za kimila.

Isadifu hapa basi kujiuliza swali moja. Je ni nani katika kipindi cha chama kimoja kushika hatamu aliweza kutofautisha kati ya Mwenyekiti wa Kijiji na Mwenyekiti wa CCM kimadaraka?

Suala la nani ana haki kati ya mmiliki wa ardhi kimila na mwenye hati, lilijotokeza tena katika Shauri la **Mwalimu Omari Vs. Omari Bilali (1990).** Wakati Mahakama Kuu ilipoamua kuwa umiliki wa aina hizo mbili katika eneo lililotangazwa kuwa la mipango miji, hauwezi kwenda pamoja na hivyo yule anayemiliki kimila hawezi kuwa na haki sawa na mmiliki wa hati.

Mashauri hayo mawili yalifanyika kabla ya ujio wa Sheria za ardhi za Mwaka 1999. Hivyo kimsingi hivi sasa si Sheria, kwani Sheria za Ardhi za Mwaka 1999 zinatambua hadhi sawa kati ya miliki hizo. Cha msingi ni kufuatia taratibu zilizowekwa ili kupata miliki husika, na kutimiza masharti katika matumizi ya ardhi husika.

HAKI ARDHI

# ARDHI NI UHAI



*Wananchi wa kijiji cha Twatwatwa wilayani Kilosa wakifuatilia kwa makini mafunzo ya sheria za Ardhi yaliyofanyika hivi karibuni chini ya uratibu wa Haki Ardhi.*

**Anuani/Ofisi**

Taasisi ya Utafiti na utetezi wa Haki za Ardhi **(HAKIARDHI)**, Sinza Mori mkabala na Mole Bar, S.L.P. 75885, DSM, Tanzania. Simu +255 22 2771360 /Faxi +255 22 2771362, +255 748 646 752.
E-mail: info@hakiardhi.org Tovuti: www.hakiardhi.org



*Washiriki wa Kongamano juu ya Haki ya Ardhi kwa wazalishaji wadogowadogo lililofanyika hivi karibuni wakiwa katika picha ya pamoja Kurasini jijini Dar es Salaam.*